

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621**


**KISWAHILI**

**Muda: Saa 3**

**Jumanne, 07 Mei 2019 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenyе jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



## **SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Ainisha mambo manne atakayozingatia mwalimu katika upangaji wa mada za muhtasari katika Azimio la Kazi.
2. Eleza maana ya dhana zifuatazo, kisha toa misano miwili kwa kila moja:
  - (a) Vivumishi
  - (b) Viwakilishi
3. Eleza kwa kifupi sifa nne za kitabu cha ziada.
4. Taja sifa kuu nne za fasihi simulizi.
5. Eleza kwa muhtasari mambo manne ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.
6. Onesha sehemu kuu nne za insha.
7. Fafanua kwa kifupi mambo mawili yanayopaswa kuoneshwa na mwalimu baada ya kufundisha katika vipengele vifuatavyo:
  - (a) Tathmini
  - (b) Maoni.
8. Orodhesha vipengele vinne muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko.
9. (a) Eleza maana ya malengo mahsus.  
(b) Taja sifa tatu za malengo mahsus.
10. (a) Eleza maana ya stadi ya kuandika.  
(b) Onesha aina mbili za mwandiko unaofundishwa katika shule za Msingi.

## **SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Fafanua manufaa sita ya kufundisha na kujifunza vitendawili kwa wanafunzi wa shule za msingi.
12. Andika insha yenye maneno yasiyopungua 300 kuhusu “Manufaa ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.”
13. Kwa kutumia mifano, bainisha tofauti na uhusiano uliopo katí ya jazi za aina za maneno zifuatazo:
  - (a) Nomino na vivumishi
  - (b) Vitenzi na vielezi
  - (c) Vivumishi na viwakilishi

## **SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

14. Eleza faida sita za kutumia mbinu ya kazimradi katika kitendo cha ujifunzaji na ufundishaji.
15. Fafanua mbinu tano atakazotumia mwalimu katika kufundisha msamati katika shule ya msingi.
16. Bainisha matumizi sita ya ubao wa kuandikia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.